Ukulima Bora wa Zao la Karafuu

Zanzibar ni maarufu kwa uzalishaji wa karafuu ulimwenguni kwa zaidi ya karne mbili sasa. Uzalishaji huo ulikuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia tani 35,000 mwaka 1830 na kumiliki soko la karafuu duniani kwa asilimia 90.

Iliongoza katika uzalishaji wa zao hilo kuanzia mwaka 1830 hadi 1940 kabla ya nafasi hiyo kuchukuliwa na Indonesia.

Tathmini iliyofanywa hivi karibuni ya Sensa ya Miti (Woody Biomass Survey 2013) imeonesha kwamba Zanzibar kwa sasa ina idadi ya mikarafuu 4,131,783**,** ambapo Unguja pekee ina jumla ya mikarafuu 277,196 na Pemba mikarafuu 3,854,587.

Tathmini ya mwaka 1997 ilionesha idadi ya mikarafuu 790,400 kwa Unguja na mikarafuu 5,042,700 kwa upande wa Pemba, ikifanya idadi ya mikarafuu yote kuwa ni 5,833,100.

Hii inaonesha upungufu wa asilimia 30 ya mikarafu ya Unguja na Pemba. Hivi sasa Zanzibar ni nchi ya tatu duniani kwa usafirishaji wa karafuu, inatoa asilimia tano (5%) tu ya karafuu zinazozalishwa duniani.

Hali hiyo ilitokana na Sekta hiyo ya Karafuu kwa ujumla kukumbwa na changamoto nyingi kama vile za kimasoko, uendeshaji na ukuaji wa sekta nzima. Serikali kwa kuzingatia umuhimu uliopo katika sekta hiyo, ilifanya tafiti mbalimbali ili kuweza kutatua changamoto hizo.

Matokeo ya tafiti hizo zilipelekea kufanywa kwa mapitio ya Sheria zinazohusika na zao la karafuu. Matokeo yake ni kupitishwa kwa sheria mpya ya ZSTC Namba 11 ya mwaka 2011, kupitishwa kwa Sheria Namba 2 ya Maendeleo ya Karafuu ya mwaka 2014 na kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu ikiwa ni miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuimairisha zao hilo.

Je kwa upande wa Wakulima wa zao hilo la karafuu wanatakiwa kufanya nini kuunga mkono juhudi hizo za Serikali za kuimarisha zao hilo kwa uchumi wa Taifa na ustawi wa Wananchi?

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC) Bi. Mwanahija Almas Ali, akimkabidhi zawadi mmoja kati ya Wakulima bora.

Ili kuhamasisha Wakulima katika kuimarisha zao hilo, Shirika la ZSTC limeanzisha mashindano ya Wakulima na Wauzaji bora wa zao hilo ambapo kila Wilaya lazima apatikane Mkulima mmoja na Muuzaji mmoja bora ambapo huzawadiwa.

Je ni zipi Sifa za Mkulima Bora wa zao la Karafuu?

Wataalamu wa Kilimo Bw. Badru Kombo Mwanvura kutoka Idara ya Misitu Unguja na Bw. Said Juma Ali Mkuu wa Idara ya Misitu Pemba wanatufahamisha mambo muhimu ambayo Mkulima anatakiwa ayazingatie katika kilimo cha zao la karafuu.

Ukubwa wa shamba

Inatarajiwa kuwa shamba kubwa lizalishe zaidi kuliko shamba dogo ingawa sio lazima iwe hivyo, inakisiwa kuwa shamba kubwa la karafuu ni kuanzia eka tatu (3) na kuendelea. Ukubwa wa shamba unatakiwa uende sambamba na wingi wa mikarafuu na uzalishaji wa karafuu kwa wingi.

Inatakiwa shamba liwe na mikarafuu angalau kwa asilimia themanini na tano (85%) kulingana na ukubwa wake.

Usafi wa shamba

Shamba la karafuu linatakiwa kuwa safi na lisiwe na pori litakaloathiri mikarafuu wala lisizongwe na miti itambaayo. Vile vile liwe safi juu na wala lisiwe na miti itambaayo.

Pia shamba linatakiwa kusafishwa baada ya mavuno kwa kuondoa matawi yaliokatika na kuliweka katika mazingira mazuri kwa uzazi ujao.

Mkulima anatakiwa kupalilia baada ya kuchuma pamoja na kuhakikisha vitu vyote ambavyo si rafiki kwa mikarufuu vinaondoka ndani ya shamba. Kuliacha shamba katika hali ya uchafu kunaondoa ubora wa shamba.

Upandaji wa Mikarafuu Mipya

Katika uimarishaji wa zao la karafuu Mkulima anatakiwa awe na utaratibu mzuri wa kupanda mikarafuu kulingana na ukubwa na nafasi ya shamba lake. Inapendeza kuona shamba lina mikarafuu ya umri tofauti kuanzia miaka mitatu (3), mine (4) na kuendelea.

Umbali wa mti na mti (Spacing Metre) inatakiwa iwe mita 7 kwa 9 kwa mikarafuu ya kupandwa na metre 5 kwa mabotea. Unapopanda mikarafuu kwa kuipa nafasi, unatoa nafasi kwa mazao mengine kuweza kuoteshwa na kulipa ubora shamba. Hali hiyo pia hulipa shamba uwezo wa kuwa na nafasi ya kupandwa mazao mengine ambayo husaidia katika kunawirisha na kustawisha mikarafuu.

Kuchanganya na Mazao Mengine

Mkulima wa zao la karafuu anashauriwa kupanda mazao ya muda mrefu na ya muda mfupi katika shamba lake la mikarafuu. Kufanya hivyo kunasaidia kumpa hamu na muda Mkulima kulihudumia vyema shamba lake.
Inahofiwa kuwa shamba linapokuwa na mikarafuu mitupu huwa halipati uangalizi mzuri na Mkulima anaweza kulitelekeza shamba lake kwa sababu mikarafuu huanza kuzaa baada ya miaka mine hadi mitano kwa msimu, hivyo Mkulima hukosa hamu na ari ya kulihudumia vyema shamba.

Mkulima anaweza kupanda mikarafuu na mazao mengine kama vile, mishokishoki, igililani, pilipilimanga, vanilla na migomba ndani ili kuipatia kivuli na kulipa uwezo shamba kukua vizuri na kuongeza kipato zaidi.

Ubunifu wa Mkulima

Mkulima bora wa zao la karafuu anatakiwa kuwa mbunifu wa mbinu za kulitunza Shamba lake ingawa ni Wakulima wachache wenye kulifanyia kazi suala hili. Tafiti zinaonyesha kuwa Mkulima bora ni yule mwenye kubuni njia tafauti za kulifanya shamba lake liwe bora. Mfano, kumwagilia maji na kuweka kivuli.

Kufuata njia bora na maelekezo ya wataalam katika utunzaji wa mikarafuu hulipa Shamba ubora wa hali ya juu.

Kukabiliana na Maradhi

Mkulima anatakiwa awe na uwezo wa kukabiliana na maradhi ya mikarafuu kwa kushirikiana na wataalamu wa kilimo. Japokuwa tafiti zinaonesha ni mikarafuu michache inayopatwa na maradhi, lakini mabadiliko ya tabia nchi imekuwa ni changamto kubwa kwa ustawi wa mikarafuu. Wakati wa kiangazi mikarafuu mingi hasa midogo hukauka kutokana na uwepo wa jua kali na joto.

Mbinu bora zinazotumika katika utunzaji wa mikarafuu

Pia tatizo jengine ni *Mlangamia* ambao hauna dawa zaidi ya Mkulima mwenyewe kuisafishia mikarafuu yake. Mkulima anashauriwa kuziona taasisi za kilimo au Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu pindi anapogundua matatizo katika mikarafuu yake ili waweze kufanya utafiti kugundua tatizo na kulitafutia ufumbuzi.

Ujenzi ndani ya Shamba.
Mkarafuu ni mti wenye maringo na nongwa na hauhitaji usumbufu katika ukuaji wake. Unaweza kujenga kibanda au nyumba moja kwa ajili ya uangalizi wa shamba lakini si vyema kukata viwanja na kujenga nyumba za maakazi ya familia.

Ujenzi katika mashamba ya mikarafuu unaondoa ubora wa shamba.

Kuwepo kwa makaazi ndani ya shamba la mikarafuu ni chanzo cha kufa na kudhoofika kwa mikarafuu kutokana na shughuli mbalimbali zinazofanywa na binadamu.

Umiliki wa shamba.
Shamba bora ni lile linalomilikiwa kihalali/kisheria na Mkulima. Ni lazima liwe na hati ya uthibitisho wa umiliki wake ili kuondoa migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza mara baada ya kupanda kwa thamani ya zao la karafuu.

Shamba bora la mikarafuu

Umiliki wa shamba unaweza kuwa wa kukodi, kuazimwa ama kupewa na serikali, kurithi na umiliki mwengine kwa njia za halali/kisheria. Hivyo basi ili Mkulima wa zao la karafuu awe bora ni lazima shamba lake liwe na uthibitisho rasmi wa umiliki.

Makala hii inamalizia kwa kutoa wito kwa Wakulima wa zao la karafuu kuendela kushirikiana na Serikali katika kuimarisha zao la karafuu ikiwa ni pamoja na kuuza karafuu zao katika Shirika la ZSTC ili kukuza uchumi wa Taifa ambao unategemea sana upatikanaji wa fedha za kigeni na kukuza ustawi wa Wananchi wote.